**LEARNING BY EAR**

# "Mihadarati na vileo – Poromoko la jamii"

## Episode 5: " Mara juu, Mara chini"

**AUTHOR: Chrispin Mwakideu**

**EDITOR: Andrea Schmidt, Aboubakary Liongo**

**PROOFREADER: Charlotte Collins**

**List of characters by scene:**

**SCENE ONE: PROTEST MARCH BY WOMEN AT THE POLICE STATION**

- **Inspekta Tino (m, 40)**
- **Beri (f, 35)**
- **mwanamke (f, 45)**
- **wanawake 4-5 (f, 18-50)**

**SCENE TWO: JABALI AND CHAMBO OUTSIDE LIMBI HIGH SCHOOL**

- **Jabali (m, 18)**
- **Chambo (m, 30)**

**SCENE THREE: OKOSHO AND ZULA AT BAMJU'S HOUSE**

- **Zula (m, 18)**
- **Okosho (m, 18)**

- **Bamju (m, 40)**
- **Wanawake 2 (f, 16-30)**

## SCENE FOUR: BERI AND PUYANGA AT HOME

- **Beri (f, 35)**
- **Puyanga (m, 50)**

**Msimulizi (m/f)**

## INTRO:

Hujambo na karibu tena katika kipindi ukipendacho cha Noa bongo! Jenga maisha yako. Leo ni kipindi cha tano katika tamthilia hii ya ubadirifu wa mihadarati kwa jina, **“ Poromoko la jamii”.** Kwa wale wageni wanaojiunga nasi kwa mara ya kwanza: katika makala yaliyopita, Okosho na Zula waliajiriwa na Bamju kuuza mihadarati shuleni. Chambo alizungumzia kuhusu hatari za mihadarati katika shule ya Limbi, ambapo Jabali rafiki wa Okosho na Zula alihudhuria. Pia kuna kiasi kikubwa cha mihadarati kilichowasili bandarini, mwenyewe akiwa ni Puyanga mumewe Beri. Mambo yanazidi kupamba moto. Wiki mbili zimepita tangu haya yote – Je hadithi itatufikisha wapi? Kaa nasi ili ujue katika kipindi cha leo kiitwacho **“Mara juu, mara chini.”** Tunaanza na mgomo usio wa kawaida katika kituo cha polisi.

## SCENE ONE: PROTEST MARCH BY WOMEN AT THE POLICE STATION

1. **SFX: POLICE SIRENS RING THROUGH THE AIR**

2. **WAKE:** **(A chorus of chanting)** Twataka mabwana wetu!

3. **INSP. TINO:** **(talking though a megaphone)** Kina mama wa Chunga Sana, kile munachotaka ni vigumu sana kufanyika. Wanaume wote walio hapa ni wahalifu.

4. **WAKE:** Afisa, hatuna haja na mahabusu katika seli zenu? Tatizo letu ni hawa wanaume wetu ambao wameshindwa kutupa haki zetu za kindoa!

5. **WAKE:** **(Same chorus of chants and ululations)**

6. **INSP. TINO:** Sijawaelewa?

7. **WAKE:** **(with emphasis)** Waume wetu hawafai tena, bure kabisa.Yote kwa ajili ya pombe haramu, kazi yao ni kuketi na kunywa, wakifika nyumbani wako chakari hawajifai hawatambui kama tunahitaji kuishi, na pia hawatupatii haki yetu ya kindoa….

8. **INSP. TINO:** Hayo ni maswala ya kinyumbani. Hatutahusiki na –

9. **WAKE:** **(interrupting)** Nyinyi ndio mumesababisha haya yote! Munashindwaje kuwashika watu wanaouza pombe haramu ! sasa vijana wetu wanawaiga baba zao!

10. **(WOMEN GRIEVE AND WAIL LOUDLY)**

11. **INSP. TINO:** **(defeated)** Bi. Beri, hebu zungumza nao…sijui nitawaambia nini tena...

12. **BERI:** **(takes megaphone and shouts emotionally)** Twataka mabwana wetu!

13. **WAKE:** **( CHANT RISES SEVERAL TIMES )**

14. **INSP. TINO:** **(shocked)** Kamishna Beri!

15. **MSIMULIZI:** Inspekta Tino hakuamini macho yake. Afisa wake mkubwa Beri kaungana na wanawake wengine kwenye maandamano! Lakini ni nani atamlaumu? Alihisi uchungu kama wanawake wengine, alishuhudia mumewe akilowa kwa pombe! Kwengineko, Okosho na Zula sasa wanaishi maisha tofauti, kwani wanalipwa bunda baada ya kuwauziya wanafunzi mihadarati. Wasichofahamu ni kuwa, hata wao, pia wameanza kuwa waathirika wa madawa hayo. Lakini kwanza, hebu tuungane na Jabali, ambae ametoka muhadhara wa pili wa mihadarati katika shule yake ya kitambo, na amemfuata Chambo nje.

## SCENE TWO: JABALI AND CHAMBO OUTSIDE LIMBI HIGH SCHOOL

16. **SFX: HIGH SCHOOL AMBIENCE IN BACKGROUND**

17. **JABALI:** **(calling out)** Samahani, Chambo! Dakika moja tafadhali.

18. **CHAMBO:** Nakukumbuka … wewe si ni mmoja wa wale vijana muliozuiwa kuingia kilabu 2000 hivi punde? Wewe na wenzako wawili?

19. **JABALI:** Ah, usinikumbushe huo usiku. Chambo, sijui walinipa nini. Sikujitambua, sikujua nilipo, au hata ni saa ngapi. Ni kama niliyepoteza fahamu.

20. **CHAMBO:** Kwa kweli, hivyo ndivyo mihadarati hufanya kazi. Hugeuza akili na hata ukakosa kufikiria vyema, kuona vyema, kutoweza kujiamulia vyema, au hata kukugeuza tabia.

21. **JABALI:** Sikujua, kweli leo nimejifunza mengi. Ndiposa naona kuna haja ya kuwanasua marafiki zangu. Tumekuwa pamoja tangu utotoni – Nimewajua maisha yangu yote. Nisingelipenda waangamie kwa kufuata njia hii.

22. **CHAMBO:** Unaweza kutaka waache kutumia mihadarati. Lakini uamuzi ni wao wenyewe. Nakumbuka mara kadhaa nilipokaa peke yangu na kujutia yale niliyoyafanya, sikuwa na matarajio. Nilisali huku nikilia kwa sababu ya kutumia mihadarati. Lakini unajuwa nini? Bado nilijikuta nikitafuta dozi zaidi.

23. **JABALI:** Baada ya kuvuta bangi na kunywa pombe, nilihisi matatizo yangu yamekwisha. Nilipata utulivu, hata nikaburudika. Lakini baada ya saa chache… Mungu wangu! Ilikuwa zahama!!!

24. **CHAMBO:** Utumiaji wa mihadarati huanza na kujaribu. Unajaribu sababu marafiki zako wanatumia. Wengine hutumia kujiburudisha, wengine kuepuka matatizo. Mwanzoni, kileo hicho chaweza kukupendeza, ndipo unaanza kutumia kila wakati. Mwisho unakuwa huwezi kuishi bila madawa hayo. Una bahati umegundua shida mapema. Wengi hufa, au kugonjeka; kupata madhara ya kudumu, au familia zao kuvunjika.

25. **JABALI:** **(takes a deep breath)** Kuna njia zozote zakuwasaidia Okosho na Zula? Ninawahofia mno.

26. **CHAMBO:** Samahani – kwa kukupa habari mbaya tupu. Lakini Habari njema ni kuwa utegemezi wa madawa unaweza kutibika. Ukipata msada na matibabu utarudia maisha yako ya kawaida. Hebu nitazame – mimi ni mfano ulio hai! Isitoshe, hiyo ni njia moja ya kutatua jambo hilo. Pia tunafaa kuzuia usambazaji wa mihadarati ile iwe nadra kupatikana , na tuelimishane kuhusu ubaya wa mihadarati hii. Hiyo ndiyo ajira yangu.

27. **JABALI:** **(enthusiastic)** Unahitaji mfanyi kazi wa kujitolea? Nimemaliza mitihani yangu, bado nasubiri kwenda chuo.

28. **CHAMBO:** Vyema kabisa! Karibu Youth Watch. Tukutane afisini kwangu kesho asubui. Lazima unaifahamu – ni kituo cha basi cha Chunga Sana.

29. **JABALI:** **(laughs out loud)** Wacha mzaha, Chambo.

30. **CHAMBO:** **(serious tone)** Sio mzaha! Tuonane hapo kesho asubui.

31. **MSIMULIZI:** Na Jabali aliachwa amesimama hapo, na maswali mengi kuliko majibu. Ni muda mfupi tu amejifunza kutoka kwa Chambo, kuhusu mihadarati. Mbona shirika muhimu kama hilo likose afisi? Hakutanabahi Jabali kuwa hatua chache tu kutoka pale alipo, Okosho na Zula walikuwa wakielekea nyumbani kwa jambazi Bamju, kumpelekea mauzo ya siku.

**SCENE THREE: OKOSHO AND ZULA AT BAMJU'S HOUSE**

32. **BAMJU:** Enhe, leo biashara vipi?

33. **OKOSHO:** Hii kitu safi sana yaani inanunuliwa sana! Karibuni tutakuwa mamilionea!

34. **SFX: BAMJU COUNTS NOTES AND COINS ON THE TABLE (STUDIO)**

35. **BAMJU:** Kazi nzuri, vijana. Leo nina zawadi yenu, mbali na mishahara yenu. Nyongeza ndogo, kwa kazi nzuri. **(shouts out)** Warembo! Njooni!!!

36. **(TWO LADIES GIGGLING AND MUMBLING)**

37. **BAMJU:** Sasa, munasemaje?

38. **OKOSHO:** **(shy and embarrassed)** Eh… eh, sijui nisemeje… waonaje Zula?

39. **ZULA:** Naona warembo wako safi, mameni!

40. **BAMJU:** Bam bam! Warembo, tafadhalini jiungeni nasi. Wacha nilete mabomba karibu. Wacha tupate brown sugar kiasi kabla ya kujivinjari, ukijidunga hii utajihisi uko peponi.

41. **MSIMULIZI:** Haya ndiyo maisha Okosho na Zula waliokua nayo, kwa mukhtasari. Maisha yaliyojaa hatari, inayowaelekeza kwenye mkasa. Je Chambo na Jabali watawafikia kwa wakati muafaka? Au tayari wameshaangamia? Riwaya haijakoma hapo... kwa sasa tutabaruku nyumbani jioni hiyo, Beri ameamuwa liwalo na liwe. Atamkabili mumewe, Puyanga.

**SCENE FOUR: BERI AND PUYANGA AT HOME**

42. **SFX: TV SET ON IN THE BACKGROUND - A FOOTBALL MATCH**

43. **BERI:** Puyanga. Nataka kuongea na wewe.

44. **SFX: DRINK BEING POURED INTO A GLASS (studio)**

45. **PUYANGA:** Ongea basi. Nakusikiliza.

46. **BERI:** **(emotional)** La, hunisikilizi ! unakunywa huku ukitazama runinga, Leo tu, naomba uniheshimu mimi badala ya hiyo chupa yako ya pombe!

47. **SFX: TV SET TURNED OFF AND REMOTE PUT ON THE TABLE**

48. **PUYANGA:** Haya. Natumai una jambo la maana!

49. **BERI:** Utaamua wewe. Leo nilijiunga na maandamano ya wanawake wa Chunga Sana.

50. **PUYANGA:** **(acting bored)** Kwa hiyo? Hebu jieleze mara moja. Beri, nataka kutazama mpira.

51. **BERI:** Wiki mbili zilizoisha nilifunguwa droo yako na nikaona maagizo ya mzigo unaoletwa kwa meli usiojulikana. Kazi yangu ya uaskari na muda niliotumika unaniambia mambo mawili, aidha ni mzigo unaohusika na ulinzi wa nchi au ni mali haramu.

52. **PUYANGA:** Kumbe? **(sarcastic)** Na ulichungua nini tena, mpelelezi Bi. Bond?

53. **BERI:** Kilichonishangaza zaidi ni kipaketi kilichokuwa kimebanishwa na maagizo hayo, nilikituma kifanyiwe uchunguzi na imebainika ni heroini. Ningelikukamata kitambo lakini nimekupa muda wa kuungama kwangu.

54. **PUYANGA:** Niungame kwako? Beri, kwani wewe ni mchungaji? Sikiliza – unafikiri ulipandishwaje cheo cha uaskari? Haya mambo ni makubwa. Yametuzidi mimi na wewe. Kwa hivyo nakuhusia uwachane nayo. Jifanye kipofu kabisa. La sivyo, sote tutakuwa taabani.

55. **BERI:** **(shocked)** Yani unataka kusema wewe au mtu mwengine ndiye alihusika na madaraka yangu kazini? Kwamba sikustahili?

56. **PUYANGA:** Ah, Beri, kwani wewe u dufu kiasi gani . Sisi tulikuweka hapo kwa sababu wewe ni mke wangu. Ukiwa mkuu wa polisi, tulijuwa biashara yetu itanoga.

57. **BERI:** Sisi? Sisi ni kina nani? Unawezaje kuita uuzaji wa mihadarati biashara? Huoni jinsi inavyoangamiza watumiaji?

58. **PUYANGA:** Hakuna mtu aliyewalazimu! Wanatumia kwa raha zao wenyewe. Wanapenda kutumia.

59. **BERI:** Hapana! Hawapendi – ni kwa sababu hawawezi kujizuia! Wakishaonja, wanakuwa mateka na wateja, yaani waathirika. Unajifanya hufahamu hilo. Wewe mwenyewe pombe imekutawala.

60. **PUYANGA:** **(threatening)** Sasa unavuka mipaka!

61. **BERI:** **(firmly)** Na wewe umevunja sheria! Puyanga, ninakushtaki kwa kushukiwa kuingiza mihadarati nchini, ambayo imepigwa marufuku.

62. **PUYANGA:** **(laughing sarcastically)** Usinchekeshe bibiye.

63. **BERI:** Sifanyi zihaka. Tayari nimechukua picha za maagizo hayo ya meli, na haya mazungumzo yote nimeyanakili katika simu yangu.

64. **PUYANGA:** Yani unasubutu kumshika mume wako wa chanda na pete?

65. **BERI:** La. Ninamshika muhalifu wa mihadarati. Kuanzia sasa, wewe ni mahabusu.. utakwenda kwa hiyari au nikufunge pingu?

**OUTRO:**

Puyanga aliweka pombe yake chini taratibu na kuandamana na Beri kituoni. Lakini je, kushika kwake ndio suluhisho la kuwepo kwa mihadarati? Bamju, Okosho na Zula watachukuliaje habari hizi? Pia kuna Chambo na Jabali. Ndio mwanzo mkoko waalika maua… Kugundua haya na mengineyo, usikose kujiunga nasi tena. Na ukipenda kusikiliza tena kipindi hiki, au vilivyopita kuhusu mihadarati na hoja zingine, tembelea tovuti zetu za www.dw.de/lbe Hadi wakati mwengine mara nyingine, kwaheri.